

KUWEKA MASHEMASI



Na, hilo ni, ya kwamba jambo la kwanza ni kuweka mashemasi kadha kanisani. Na kanisa letu hapa hujitawala lenyewe. Halina dhehebu lo lote wala cho chote kutuma mashemasi wake, linajichagulia mashemasi wake. Hujichagulia mchungaji wake, linachagua wadhamini wake, linachagua kila kitu kiingiacho na kiondokacho kanisani. Hakuna mtu mmoja aliye na mamlaka yote juu ya cho chote, ni kanisa. Na kanisa ni wale wajao na kulisaidia kanisa kwa kuhudhuria kwao, na kwa fungu lao la kumi na sadaka zao, ndio walio na mamlaka halisi katika kuwekwa kwa hao.

² Nami nataka kushukuru halmashauri iliyotangulia ya mashemasi, nami nasema haya hapa kwa niaba ya kanisa lote. Kama ye yote wa hao ndugu yuko hapa, ambao walikuwa Ndugu Cox, Ndugu Fleeman, na Ndugu Higginbotham na Ndugu Deatsman, wametuhudumia vizuri, wamemhudumia Bwana, katika maskani haya.

³ Na kila baada ya muda fulani, kulingana na sheria za kanisa, kila mwaka, mashemasi au wadhamini humaliza muda wao. Na kama wanataka kurudi, vema. La, hawataki kurudi, basi wanaweza kuweka wengine mahali pao, kwa kuwa halmashauri hii imejiuzulu.

⁴ Na usiku uliopita niliita halmashauri ya wadhamini, ambako kuna halmashauri mpya ya wadhamini. Nami nilimwona Ndugu Luther McDowell hapa usiku huu, tuna furaha kumwona yeye humu, aliyekuwa hapo awali kwenye halmashauri ya wadhamini. Nilienda chini kule juma hili kuona na kuchunguza na kutengeneza nakala nyingine, ambayo itatolewa kwa kanisa, pia. Basi wadhamini wa kanisa sasa ni Ndugu William Morgan, Ndugu Mike Egan, na Ndugu Banks Wood, na Ndugu Roy Roberson. Nao wote wanatoka mji huu, ila Ndugu Roberson anayeishi kati ya miji hii miwili. Bwana ameona ustahivu katika watu hao, nao wamekuwa watu wenye heshima, nao wamepokea wajibu wao kama mashemasi wa kanisa hili.

⁵ Ndiposa mkutano huu ulipokuwa ukiendelea, na niliambiwa na makamu wa mchungaji kuwa sisi . . . kuchagua halimashauri mpya ya mashemasi, ya kwamba muda wa hawa ulikuwa umemalizika na—na wamejiuzulu, na ilikuwa ni kuwachagua mashemasi wengine. Sasa, kanisa . . . Jinsi hili lifanywavyo, ni, halmashauri yaweza kuchagua mashemasi, wanaume ambao wameshirikiana nao na kuona kuwa ni watu waaminifu na wenye haki.

⁶ Afisi ya shemasi ni afisi kubwa sana, na ni heshima kubwa sana kwa Bwana kuwa shemasi kanisani. Na kwa hivyo,

mkutanoni usiku uliopita, mtu fulani alitajwa kwangu. Na tulipokutana na mchungaji, iliyofuata. . . Ijumaa hii iliyopita, ilikubaliwa na mtu huyu kuwa hawa walikuwa watu waaminifu na watu wenye haki.

⁷ Kijana mwanamume mmoja waliyempata, hakustahili kabisa (si kwa sababu yeye hakuwa mtu anayefaa), mmoja aliyetajwa na mmoja wa watu waaminifu wa halmashauri yetu ya wadhamini. Lakini mimi nilipokutana na mchungaji, na nikauliza umri wa kijana yule, alikuwa katika miaka yake ya mwanzoni ya ishirini. Mtu halisi, mwaminifu, na mwenye haki, lakini tuliona kuwa yeye alikuwa hajaoa. Biblia huamrisha shemasi awe mtu aliyeoa. Yeye sharti awe mume wa mke mmoja.

⁸ Ndiposa mwanamume mwingine ambaye ni mtu mwadilifu sana, anayestahili sana kwa kazi hiyo na angekuwa mtu mwaminifu, kama ndugu alivyomtaja. Kisha baada ya kuchunguza jambo lile, ndugu huyo alikuwa tu ameingia katika Imani hii hivi majuzi, mke wake haiamini. Basi hilo halikumstahilisha mtu yule afisi hiyo. Kwa sababu yeye lazima awe na jamaa inayotii, lazima pia wawe katika Imani, kwa sababu ingeleta mzozo.

⁹ Nasi tunajenga sasa, na tunatumai kuweka kanisa hili mahali pake. Na kama msimazi mkuu wa kanisa, lazima nione kuwa limewekwa, Kimaandiko, kila kitu kwa Neno.

¹⁰ Na hivyo basi, ndipo, imeonekana inafaa kwa halmashauri na mchungaji, wa msimamizi, kuchagua katika kundi hili la watu hapa watu fulani tunaowadhani watu wenye heshima na wenye haki. Tunaweza tu kuwaleta. Na ni, kisha, wanachaguliwa na kanisa, kwa kura zao wenyewe. Ndiposa watu hawa watatumika, kama wanajisikia kuwa watakubali afisi hii. Ndipo watakuja kwa wakati mdogo, kuona kama wanajisikia kuwa labda Mungu amewaita. Na kama baadaye, kama wanajisikia kuwa hawastahili, basi, wana haki katika majuma machache yajayo kujiuzulu afisi hii, kusudi mtu mwingine apate kuchaguliwa mahali pao.

¹¹ Walakini, mwanzoni mwa mkutano wa ufufuo ambao (kama Mungu akipenda) nataka kuwa hapa katika Maskani haya mara tu nipumzikapo, ndipo ni—ndipo ni. . . tutawaweka mashemasi hawa kwa kuwawekea mikono mashemasi na mweka hazina katika kanisa hili. Lakini kwanza hawana budi wachaguliwe na—na kuona jinsi waipendavyo na jinsi kusanyiko lipendavyo. Kisha kama ni—basi kama ni sawa pande zote mbili, basi tunawafanya watu hawa mashemasi waliochanguliwa, kama tu vile Wadhamini wanavyoteuliwa vivyo hivyo.

¹² Ni mamlaka na sheria za kanisa, kwa Neno la Mungu. Kwa hivyo, basi, hawawezi kusema kuwa “Nadhani mtu huyu angekuwa anayestahili,” hilo sivyo, “Ndugu Neville anadhani mtu huyu angefaa,” au “halmashauri ya wadhamini wanadhani

mtu huyu angefaa.” Yabidi iwe kwa kanisa! Hakuna mtu afanyaye lo lote mwenyewe hapa. Ni kura ya kanisa. Kanisa ndilo lenye mamlaka.

¹³ Fungu la kale la sheria liliharibiwa katika mafuriko ya mwaka wa 1937. Tumezinakili tena hizo, na zitatundikwa kwenye ukuta hapa hivi karibuni, wajibu wa wadhamini, mashemasi, mweka hazina, na wengineo, mchungaji, wasaidizi, na wengineo.

¹⁴ Kwa neema ya Mungu, imesemwa kwangu, na kura asilimia mia moja kupitia kwa halmashauri ya kanisa hili, kuwa wameona kuwa Ndugu Hollin Hickerson kuwa mwenye haki, mtu mwadilifu, na anayestahili cheo hiki kupokea he—heshima kuu ya kuwa shemasi wa haya Maskani yaliyotajwa.

¹⁵ Pia, tumeona, kwa kura ya halmashauri, kuwa Ndugu Collins pia ameonekana kuwa mtu mwadilifu na mtu mwenye haki. Akiwa mhudumu, mwenyewe, kwa hivyo tungemuomba aje na kuwa she—shemasi wa kanisa; na si shemasi tu, bali msaidizi wa Ndugu Neville, na labda kwa darasa la shule ya Jumapili, au kuchukua mahali pa Ndugu Neville, au lo lote analoitwa kuwa msaidizi wa Ndugu Neville. Huyu ni Ndugu Collins.

¹⁶ Na, pia, kanisa limeona, kwa kibali, ya kwamba Ndugu Tony Zable, mtu mwadilifu na mwenye haki, na amepata kibali mbele ya halmashauri ya wadhamini na wachungaji, kumuuliza achukue afisi ya shemasi katika Maskani yaliyotajwa.

¹⁷ Na pia imeulizwa, na kuonekana mtu mwadilifu kati yetu . . . (Si . . . hawa sio tu waaminifu pekee, sasa, lakini wameteuliwa tu na halmashauri.) Ndugu Taylor toka Henryville, au Memphis, naamini ni Memphis, Indiana. Yeye amekuwa nasi kwa muda, akisaidia kama bawabu na lolote lile. Kwamba amepata fadhili mbele ya kanisa hili, au halmashauri na mchungaji, kuwa yeye angekubali a—afisi kuu kuwa shemasi wa Maskani yaliyotajwa.

¹⁸ Na pia imeulizwa kuwa mkwe wa Ndugu Mike Egan, Ndugu—Ndugu Bob Harnard, ameteuliwa na halmashauri na mchungaji, kukubali afisi ya mweka hazina wa Maskani yaliyotajwa, ambayo ni kazi ya heshima, na inahitaji haki na heshima.

¹⁹ Katika kufanya hili, nadhani, ndugu zangu, ambao nawaita toka hapa, kuwa ingekuwa heshima kuu kwenu. Na si hivyo tu, bali kitu fulani cha kufanya.

²⁰ Na wakati huu nitamwita Ndugu Neville, msaidizi wetu, asome masharti ya shemasi. Ndugu Neville, kama ukiyasoma toka kwa Neno la Mungu. [Ndugu Neville asoma 1 Timotheo 3:8–13—Mh.]:

Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana, si watu wanaotamani fedha ya aibu;

Wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi.

Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia.

Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote.

Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakisimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao.

Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo.

²¹ Amina. Ningependa wakati huu kuwauliza hawa ndugu waliotajwa, kama wangekuja mbele hapa jukwaani kwa dakika chache. Nasi tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda mdogo wa maombi, nawataka... Na kanisa lajua hili ni nini, kuwa huku ni kuchagua halmashauri yenu ya mashemasi na mweka hazina wenu.

²² Bwana Yesu, ni kwa mawazo ya busara na ya kiungu tunakuja kwako Wewe sasa. Tunakuja kwa heshima ya Neno Lako Takatifu sana, tunakuja tukiamini kuwa "Na kila neno la mwanadamu liwe uongo, bali la Mungu liwe kweli." Na tuna shukuruni Kwako kwa Kanisa hili ambalo Yesu amenunua kwa Damu Yake Mwenyewe ya thamani, na ametupa sisi jengo hili tuabudie.

²³ Na kama wasimamizi wa hili kundi kuu, ambalo Roho Mtakatifu ametuchagua kusimamia, tunajaribu sasa kukabidhi kusanyiko hili kundi la watu waaminifu, na wenye haki ambao twaamini kuwa wamejazwa Roho na wako tayari kwa huduma. Kama ilivyosemwa wakati mmoja kuhusu halmashauri ya mashemasi, "Chagueni miongoni mwenu watu, walioshuhudiwa kuwa wema na walio na Roho Mtakatifu, tuwaweke juu ya jambo hili, kuwashughulikia wajane na yatinia, kugawa pesa, na kushughulika na mambo ya kanisa." Miaka ya baadaye, tumesoma tu maandishi ya mtakatifu Paulo, mtu mkuu, aliyetiwa pumzi na Mungu, aliyeweka taarifa ya Maandiko juu ya masharti ya cheo kama hicho.

²⁴ Mungu wafadhili watu hawa. Na sasa ni chaguo, Bwana, kama kanisa lenye mamlaka, kama mwili wa Bwana Yesu, ya kwamba wachague. Na [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]... na utaongoza sehemu hii ya ibada kwa njia maalum, katika hilo Jina lenye haki na takatifu la Yesu.

²⁵ Sasa hali vichwa vyetu vimeinamishwa, si vichwa vyetu tu bali na mioyo yetu, na kila mshiriki wa kanisa hili... anayekuja hapa kila mara na kulisaidia kwa fungu lako la kumi na sadaka, anayechukuliwa kama mshiriki wa kanisa hili. Hali, mchangaji

pamoja nami, pekee yetu, mchu—mchungaji msaidizi Ndugu Neville pamoja nami tukiwatazama. Ningeuliza kama kanisa hili lamwona Ndugu Taylor kuwa mtu mwenye haki na anayefaa, kwa mawazo yenu bora, kuwa shemasi juu ya kundi hili la watu? Mtaonyesha hivyo kwa kuinua mikono yenu. [Ndugu Branham atulia—Mh.] Vema. Sasa kama kunaye anayepinga, na ainue mkono wake. [Ndugu Branham atulia—Mh.] Asanteni.

²⁶ Je, ye yote wa washiriki wa kanisa hili hapa aona kuwa . . . na wote, mwamwona Ndugu Hollin Hickerson kuwa mtu mwenye haki na mheshimiwa, mtu ambaye ameonekana machoni penu kuwa anastahili kuwa shemasi wa kanisa hili lililotajwa? Onyesha kwa kuinua mkono wako wa kuume. [Ndugu Branham atulia—Mh.] Kama kunaye anayepinga na ainue mkono wake. [Ndugu Branham atulia—Mh.]

²⁷ Je, kusanyiko hili linamwona Ndugu Collins kuwa vivyo hivyo, mtu mwenye haki na heshima, na anayestahili kazi ya shemasi wa kanisa hili? Inueni mikono yenu. [Ndugu Branham atulia—Mh.] Vema anayepinga, na ainue mkono wake. [Ndugu Branham atulia—Mh.]

²⁸ Je, kusanyiko hili linamwona Ndugu Zable kuwa mtu mwenye heshima na anayestahili huduma hii ya kuwa shemasi juu ya kundi hili katika kanisa hili lililotajwa? Mnaweza kuinua mikono yenu ya kuume [Ndugu Branham atulia—Mh.] Mnaopinga, inueni mikono yenu. [Ndugu Branham atulia—Mh.]

²⁹ Je, kusanyiko hili linaonelea kuwa Ndugu Harnard ni mtu mwenye haki, ambaye amekuwa nasi kwa muda, kuwa mweka hazina, mwandishi—mweka hazina wa kanisa hili, kushika hazina zake na kulipa madeni yake? Kama ndivyo, inueni mikono yenu ya kuume. [Ndugu Branham atulia—Mh.] Ka kama kuna ye yote anayepinga, ainue mkono wake wa kuume. [Ndugu Branham atulia—Mh.]

³⁰ Napenda kusema kwa ndu—ndugu wanaosimama wakati huu, chini ya msalaba huu, kuwa kanisa hili, asilimia mia moja (hakuna aliyepinga kamwe), linaonelea ninyi nyote mnastahili machoni pa Mungu kwa afisi hii ambayo Mungu amewaitia.

³¹ Sasa, mmesema, “Hawa pia na wajaribiwe pia kwanza, na kuona kama wanataka afisi hii.” Baada ya majuma machache, Mungu akipenda, nitarudi tena kuweka mikono juu ya kundi hili la watu, kuwafanya kisheria wadha . . . au mashemasi wa kanisa hili, na mweka hazina.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika chache:

³² Bwana, tuna furaha usiku huu kuwa kuna wanadamu ambao bado wanaishi duniani wanaoweza kuenenda wakimcha Mungu mbele ya ulimwengu; wacha Mungu sana hata Maskani, yenye sheria kali kama haya, yanaweza kuwapigia kura watu watano kama viongozi wao, bila kura moja ya kupinga. Tuna shukrani

kwa ajili yao, nasi twajisikia kuwa Wewe ulikuwa pamoja nasi katika maamuzi haya, halmashauri pamoja nasi wachungaji.

³³ Mungu, uwabariki watu hawa. Na wao watumikie afisi hii kwa mioyo yao yote, wakijua kuwa inawanunulia baraka kuu Mbinguni. Siku moja Vitabu vya Mbinguni vitakapofungwa, na kile Kitabu cha viumbe wa kimbinguni na wakati kile Kitabu kikuu cha Mbinguni kitakapofunguliwa, majina yao na yawe asilimia mia moja mbele za Mungu na Mwokozi na mbele ya majeshi yote ya Mbinguni, yawe vivyo hivyo katika Ufalme wake. Uwabariki, Bwana, nao na watumikie afisi hii vema. Katika Jina la Yesu twakushukuru Wewe kwa ajili yao. Amina.

³⁴ Nataka tu kusalimiana nanyi kwa mikono. [Ndugu Branham asalimiana nao kwa mikono—Mh.] Ndugu Harnard, na Ndungu Zable, na Ndugu Collins, Ndugu Hickerson, na Ndugu Taylor. Furaha tele kujua kuwa tumekuwa tukishiriki wakati huu wote na watu waaminifu kama hawa. Mungu awabariki sasa. Nasi tutawaona hivi sasa, mara nipumzikapo kidogo na kurudi, na kuona jinsi mnavyopenda afisi yenu. Vema, kwa kura zao, nadhani ilikuwa asilimia mia moja, hakuna iliyopinga hata moja.

³⁵ Jamani, si mna furaha kuwa mnashiriki na watu siku hizi wanaoweza kuishi mbele za Mungu, wacha Mungu, na kuishi mbele za huu ulimwengu wa sasa katika hali hiyo? Ni jambo la ajabu.

³⁶ Nami nina furaha sana kujua usiku huu kuwa nimejaliwa ku—kuwa na watu hawa na kanisa hili kama marafiki wangu. Nina furaha sana kuwa Mungu aliniruhusu kushirikiana na Kanisa Lake kote ulimwenguni. Lo, wanadharauliwa na kukataliwa na kunenwa, na kama nilivyosema asubuhi hii katika ujumbe wangu, labda wagaaga matopeni, jinsi ulimwengu uwaonavyo, kama “kundi la wakithiri dini,” lakini Mungu awaona wao kama watoto Wake. Nina furaha sana kwa ajili ya hilo. Huenda wasiweze kuwaambieni ni maili ngapi hata mwezeni. Huenda wasiweze kuwaambieni sayari zote na jinsi zinavyotenda kazi. Lakini kuna kitu kimoja wanachojua, wanajua saa waliyozaliwa mara ya pili. Nina furaha tele kwa ajili yao.

³⁷ Na kama mfano mdogo niliojifunza, nami nitautumia usiku huu kwa wasichana wangu wadogo wawili ili ipate kueleweka vizuri sana kwetu sisi, kulifanya halisi kwetu sisi, mpate kuelewa maana yake. Asubuhi moja nikiamka toka kitandani. . . Nina wasichana wadogo wawili. Mmoja wao ni Rebeka na mwingine ni Sara, nao ni wasichana wadogo wa baba.

³⁸ Nami nina mvulana mdogo, Joseph. Nami nilikuwa natoka Chattanooga, toka mkutanoni usiku mmoja, nilipokuwa huko katika mkutano huu wa mwisho. Nami nilikuwa ka—katika motokaa, nikisafiri na mwanangu mkubwa, Billy. Mke wake

na Meda walikuwa garini, na hao wasichana. Na tulipokuwa tukisafiri njiani, hakuna aliyekuwa amenena cho chote kwa urefu wa nyumba kadha za mji. Nami nilikuwa nimewakemea watu sana usiku huo kuhusu waliyokuwa wakifanya. Na hakuna ye yote aliyekuwa amesema lo lote. Na maskini Joseph akaja na kunishika mabegani, yeye akasema, “Baba, umehubiri kweli kweli usiku huu!”

³⁹ Na asubuhi hii, nilipokuwa nikiondoka kuelekea Barabara ya Nane na ya Kumi, ile... au ya Penn na ya Kumi, samahani, hakuna mtu alikuwa amesema jambo lo lote, mke na hao wasichana wawili. Na maskini mtoto Joseph akashika mabega yangu tena, akasema, “Baba, hayo, hakika nilipenda sana mahubiri hayo asubuhi hii,” yeye akasema.

Nilisema, “Vema, nina mshabiki mmoja, huyo ni mwanangu.”

⁴⁰ Na kwa msemu wetu mdogo. Nalipoamka asubuhi moja, nikiketi chumbani, maskini Beky alikimbia akaja na, kasema, alinikalia mguu mmoja na kunikumbatia, naye ni msichana wa babaye. Naye alikuwa akinikumbatia. Na maskini Sara akaruka toka kitandani amevalia nguo zake za kulala na angekuwa, tuseme, aliyefuata kwa kukimbia. Yeye ni mdogo na mwenye macho ya rangi ya kahawia.

⁴¹ Maskini Beky angesema, “Ee, Sara, huna haja kuja, kwa sababu baba ni wangu mimi pekee. Baba ni wangu wote!” Na maskini Sara, midomo yake ilikunjamana, macho yake madogo ya rangi ya kahawia yakafungamana. Nilitoa ishara hivi na kukunja goti lingine, naye akaja na kulikalia.

⁴² Beky ana miguu mirefu zaidi, kwa hivyo angefikia sakafu. Maskini Sara alikuwa akibatabata, kwa hivyo nikamshika Sara kwa mikono yote miwili. Maskini Sara akamtazama Beky na kusema, “Beky, huenda ukawa na baba wote, lakini baba ana mimi wote!”

⁴³ Nami nadhani ndivyo ilivyo hapa. Huenda tusijue theologia yote, tusijue maneno yote makuu ya Kiyunani, hili kundi la watu huenda lisijue. Lakini kuna moja dhahiri, naamini Yesu ana *sisi* sote. Amina.

Vema, Ndugu Neville.



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org